



CITY OF BUFFALO  
DEPARTMENT OF PERMIT  
AND INSPECTION SERVICES  
65 NIAGARA SQUARE, ROOM 324  
BUFFALO, NY 14202

BAR CODE  
FIRSTNAME LASTNAME  
1234 ADDRESS AVENUE  
BUFFALO, NY 14202

## GET AHEAD OF LEAD

Mpendwa Mmiliki wa Mali ya Kupangisha,

Kama mmiliki wa mali ya kupangisha katika City of Buffalo, unahitajika kuchukua hatua mahususi ili kulinda mali yako dhidi ya madini ya risasi. Kulingana na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, watoto walio kwenye hatari ya madini ya risasi wanaathiriwa maisha yao yote kwa werevu wa kiwango cha chini, kupoteza uwezo wa kusikia na ulemavu wa kujifunza. Sumu ya madini ya risasi mara nyingi husababishwa na vumbi kutoka kwenye rangi ya madini ya risasi, haswa katika nyumba za kupangisha.

City of Buffalo ni mshirika katika Get Ahead of Lead, mradi wa kusaidia wamiliki wa mali kufuata sheria za ndani na Serikali Kuu zinazozuia sumu ya madini ya risasi. Tunakuhimiza utembelee [www.getaheadoflead.org](http://www.getaheadoflead.org) ili ujifunze mengi kuhusu hatua unazopaswa kuchukua ili kulinda mali yako dhidi ya madini ya risasi. Soma nyuma ya karatasi hii ili ujifunze zaidi kuhusu vyanzo vya sumu ya madini ya risasi na desturi za kazi salama za madini ya risasi.

Asante kwa kutekeleza wajibu wako wa kutunza watoto wako kwa afya njema na kuwalinda.

Wako mwaminifu,

James Comerford  
Kamishna, Idara ya Huduma za Kibali na Ukaguzi  
(Department of Permit and Inspection Services)



Taarifa hii ya kuelimisha inaelezea hatari za madini ya risasi nyumbani kwako na mali ya kupangisha.

## TATIZO NI NINI?

- Vumbi la rangi ya madini ya risasi ni chanzo kikuu cha sumu ya madini ya risasi utotoni nchini Marekani
- Vumbi la rangi ya madini ya risasi katika nyumba zilizojengwa kabla ya 1978
- Buffalo ina nyumba za zamani sana nchini Marekani. Zaidi ya asilimia 90 ya nyumba zilijengwa kabla ya 1978

## KWA NINI HILI NI MUHIMU?

Sumu ya madini ya risasi inaweza kusababisha:

- Uharibifu wa Ubongo Milele
- Ulemavu wa Kusoma
- Kupoteza Uwezo wa Kusikia
- Ugonjwa wa Moyo
- Kuharibika kwa Mimba na Kujifungua Kabla ya Wakati

## NINAWENZA KUFANYA NINI?

Wamiliki wa mali, meneja na wenye nyumba wanaweza kuzuia sumu ya madini ya risasi kwa kuhakikisha kuwa desturi salama za madini ya risasi zinatumiwa wakati wa marekebishi na kupaka rangi vifaa.

1. Usivuruge sehemu zilizopakwa rangi ambazo ziko katika hali nzuri.
2. Ikiwa sehemu ina rangi inayoambuka, piga simu 311
3. Hudhuria darasa kuhusu marekebishi salama ya madini ya risasi na desturi za ukarabati | Jisajili kwenye work.leadSAFE@erie.gov au piga simu 716-961-7582
4. Tumia desturi za kazi salama za madini ya risasi wakati unarekebisha, kukarabati au kupaka rangi nyumba yako au nyumba za kupangisha



KWA MAELEZO  
ZAJIDI

PIGA SIMU  
TEMBELEA

311  
www.getaheadoflead.org

### Erie County Department of Health

- Cheti / Kozi ya RRP
- Ruzuku kwa wamiliki wa nyumba
- Ruzuku kwa wenye nyumba
- Rasilimali Nyingine

Simu: 716-961-7582

Barua pepe: work.leadSAFE@erie.gov

### City of Buffalo

- Ukaguzi na Vibali vya Nyumba
- Usajili wa Upangishaji
- Fomu ya Ilani ya Rangi ya Madini ya Risasi / Fomu ya Uthibitishaji wa Madini ya Risasi
- Rasilimali Nyingine

Simu: 716-851-5227

Barua pepe: leadSAFE@city-buffalo.com

Lugha Nyingine  
Zinapatikana Ukiomba.  
Piga Simu  
716-851-5227